

# Siku *Ya* Maombi *Kwa Ajili Ya*

# Amani *Ya* Yerusalemu

# JumaPili ya Kwanza ya Kila Mwezi Wa Octoba

**Mambo Muhimu kuhusu Siku Ya Maombi Kwa Ajili Ya Yerusalemu**

## HIKI NI NINI?

**Siku ya kimataifa ya Maombi Kwa Ajili Ya Amani Ya Yerusalemu,** iliasisiwa kwa uthibitisho wa ZAIDI ya viongozi wa Ki-kristo 1200 toka madhehebu na tamaduni mbali mbali za ulimwengu, tukio litakalojiri kila Jumapili ya kwanza ya kila mwezi wa Octoba.

**Wito wetu wa kutegemeza, kwa wenye nia hiyo, wana maombezi walioarifiwa kote duniani kwa mipango na makusudi ya Mungu kwa ajili ya Yerusalemu na watu wake.** Uasisi wa awali wa maombi duniani umerandana kwa majira ya Yom Kippur , na kwa mara ya kwanza katika historia ya kanisa, hutengeneza juhudi katika kufikiria kalenda ya lutulujia ya Ki-kristo na Ki-biblia, sawia na kalenda ya Ki-yahudi.

**Huu Uasisi wa Maombi ya Ki-limwengu uko chini ya mwenyekiti-mwenza Dr. Jack** Hayford (Rais wa The Foursquare Church na Mkurugenzi wa The King's College & Seminary) na **Rev. Robert Stearns** (Muasisi na Mkurugenzi wa Huduma za Eagles' Wings )

## LINI LIFANYIKE?

Siku ya Maombi Kwa Ajili Ya Amani Ya Yerusalemu itatekelezwa kila Jumapili ya kwanza ya kila mwezi Octoba, kwa uwiano wa majira ya Yom Kippur. Mwaka huu – ***2010 – siku hii itaangukia tarehe 3 Octoba.***

## WASHIRIKI NI KINA NANI?

- Makumi ya mamilioni ya Wakristo, toka kote katika tamaduni, madhehebu na vizazi toka makanisa makuu kwenye miji ya ki-limwenguni kote hadi ngazi ya makanisa ya chini yaliyoezekwa kwa nyasi katika Afrika na hata yale yaanzayo kwa viwango vya chini katika mataifa ya Ki-islamu.

- Mwaka 2009 tulikuwa na takribani mataifa 175 yaliyoshiriki – **ambayo miongoni mwao ni pamoja na makanisa 7 yaliyoanza kwa viwango vya chini toka mataifa ya Ki-islamu** – na katika mwaka huu 2010, kwa neema ya Mungu, tunaamini kuwa na zaidi ya mataifa mengi yatakayoshiriki katika kuomba kwa ajili ya Amani ya Yerusalemu.

## NI NAMNA GANI SIKU HII MUHIMU INATAZAMIWA?

- *Ki-msingi, kuomba kwa ajili ya amani ya Yerusalemu yapaswa kufanyika katika ibada za kanisa la mahali kama sehemu ya huduma za ibada zao katika mwezi Octoba tarehe 3. Kushiriki katika DPPJ katika ibada ya mahala yaweza kuwa kwepesi ili mradi hapakusahaulika matumizi ya vipeperushi au matangazo mafupi ya DPPJ kwa kanisa katika programu zao, na kushirikisha jumbe & baadhi ya maombi yasisitizayo kulihusu jambo hili siku ya Octoba 3, au, lililojumuisha muda utakakaotumika kama likusidiaivyo kanisa Fulani kutenda. Kilicho, cha muhimu zaidi ni kuwa tunahitaji kila aina ya makanisa, toka katika kila mkabala wa ki-ibada, toka kote Marekani, waungane na wa-Kristo ulimwenguni kote kuomba kwa ajili ya Amani ya Yerusalemu, kwa kiwango chochote kile kwa kuelewa kuwa wanalo jukumu juu ya hitaji hili tanzia.*
- *Baadhi ya miji, nchi au mataifa pia wawe na makusanyiko ya majimbo – kama nyongeza katika huduma za ibada za kanisa la mahala – yaani, wadhihirishe umoja wao katika maombi ya amani ya Yerusalem na watu wake.*
- *Ipo Siku ya kipekee ya kusanyiko la Maombi Octoda 3 Yerusalemu, yakiweka pamoja viongozi wa Makanisa toka kote ulimwenguni na watu wa Israeli walio mahiri ambao watarushwa moja kwa moja katika God TV kwa zaidi ya mataifa 200 siku hiyo.*
- *Kadhalika, papo masaa 24 ya maombi ya mdahalo kwa njia ya simu, yatakayoendeshwa na Greater Calling (www.greatercalling.org) ambapo watu toka pande zote za dunia, kwa tofauti za masaa ki-kanda, wanaweza kujikuta katika chumba cha maombi ya" ana kwa ana" kupitia simu zao na kuomba pamoja kwa ajili ya mahitaji mbali mbali ya mikakati ya jimbo na watu wa makundi husika.*

## NAWEZAJE KUPATA TAARIFA ZAIDI?

Tafadhali, tembelea www.daytopray.com kwa yafuatayo:

- Tafsiri ya zana za Siku ya Maombi, peperushi, jumbe, nk. Katika lugha mbali mbali, zinazoweza kuchukuliwa katika mtandao &/au kuzalishwa toka katika kompyuta yako. Tunavyo vitendea kazi au zana zilizotafsiriwa katika lugha mbali mbali 19 katika tovuti yetu tangu mwaka jana na yataboreshwa na kuendeleza tafsiri mwaka 2010.
- Tayari zipo zana kwa ajili ya watoto zinazoweza kuchukuliwa toka katika mtandao kwa ajili ya Programu za watoto wa DPPJ wa miaka 3 – 6, na wa miaka 4 – 10. Hii ni pamoja na masomo, staidi za mikono, kurasa zilizonakshiwa kwa rangi, na kadi nzuri za maombi.
- Tunapanga kuwa na Programu ya Vijana wa DPPJ kwa ajili ya vijana walio chini ya umri wa miaka ya utata na, iliyo tayari katika mtandao na ratiba za huduma mbali mbali, maigizo mafupi, jumbe, vidio, na muziki.
- PSAs (Huduma ya Matangazo kwa Wengi) katika sauti na mfumo wa Vidio
- Machapishi/Matoleo ya Habari.
- Orodha ya viongozi walioridhia wito wa maombi toka kote duniani

- Orodha ya Mataifa, Waratibu-wahamasishaji wa Ki-taifa, na Ki-mataifa kwa ajili ya mwenendo wa maombi, haya yakiwa pamoja na namna ya kuwasiliana nao kwa maswali.
- Vyanzo na nyenzo zinavyoweza kuagizwa ili kulikamilisha kanisa lako au kikundi cha wasoma Biblia au kwa ajili ya kuiwezesha siku yako ya maombi Octoba 3
- Picha na maelezo ya ufuatiliaji wa miaka iliyopita kiutendaji.
- Historia ya Siku Ya Maombi Kwa Ajili Ya Amani Ya Yerusalemu

Waweza pia kuwasiliana nasi kwa simu na Ofisi ya Eagles' Wings kwa nambari 716-759- 1058 or

1-800-51 WINGS

## NAMNA GANI NAWEZA KUSHIRIKI?

Unaweza kuwasiliana na mratibu wa jimbo lako, nchi au taifa  kwa kupitia webpage ya uratibu wa DPPJ ambapo unaweza kututumia barua pepe moja kwa moja kwa kuungana nao kwa majina husika.

Iwapo taifa, jimbo, au nchi yako haina Mratibu wa DPPJ, basi waweza kuwasiliana nasi kwa kupitia tovutu yetu www.daytopray.com au kwa kutupigia simu yetu ya ofisini namba 1-800-51 WINGS.

## JE, KUOMBA KWA AJILI YA AMANI YA YERUSALEMU KUNA MAANA YA KUWA KINYUME CHA WAARABU NA WAPALESTINA?

Mungu si mwenye kumheshimu mwanadamu;  na kwa usawa anampenda kila mtu. Anao mpango wa ukombozi kwa uzao wa Isaka na uzao wa Ishmaeli. Tunapoomba kwa ajili ya Amani ya Yerusalemu, hivyo tunaomba kwa ajili ya watu wote waishio mahala pale. Mioyo yetu ni kuliona neno la Mungu likikamilishwa. Tunataka kuona ukuta wa matengano kati ya Wayahudi na Waarabu ukivunjwa (Efeso 2:14), kuona ushirikiano, upendo na shukrani kwa mrejeshwa, na utele wa amani (Shalom) ya Mungu na baraka vikitulia juu ya nchi na watu wake.

## KWA NINI NIOMBE KWA AJILI YA AMANI YA YERUSALEMU?

- **Mwanzo 12:3 –***Bwana anasema katika agano aliloliweka na Abraham:*

  ***"Nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa." Kwa uwazi zaidi, Historia inabaini kuwa mataifa hayo na viongozi waibarikio Israeli na Wayahudi walibarikiwa na Mungu, na wao wawalaanio Wayahudi  na Ardhi yao Takatifu, wao wenyewe wamejitia kitanzi cha ghadhabu ya Mungu.***

- **Mungu aliwavuvia waandishi wa maandiko kuwatakia baraka isiyo na mipaka wote wamfuatao na kulitenda neno lake *"Utakieni Yerusalemu amani; na wafanikiwe wakupendao;"* *(Zaburi 122:6)*.**

- ***Yerusalemu – na taifa la Israeli –ndiyo pekee demokrasia (yenye uhuru wa kidini na haki kwa watu wote kwa jinsia zao) kwa ukubwa wa mataifa 22 ya Uarabu yasiyo jamaa.*** *Israeli na Marekani daima huitetea heshima hiyo na uhuru kinyume na adui yule aliyezoeleka…. Yaani Islamu yenye siasa kali na mrengo wa kushoto.*

- **Tuna wiwa deni la shukrani kwa Wayahudi, deni iliyo kubwa kupita kiasi kwa kuwa kwao, msingi wa imani yetu ya Ukristo na mchango wao usio na kipimo katika kuiinua jamii kwa vumbuzi za madawa, kilimo na maendeleo ya teknolojia.**

- **Ni wajibu wa kanisa kusimama na watu wote wa agano kwa ajili ya urejesho wa Israeli na makusudi ya Mungu katika nchi hiyo.** ***Ni wajibu wa Wakristo Kuukamilisha Unabii wa Mungu kwa wayahudi katika kizazi chao.***

- **Historia ya Kanisa inabaini sana mateso dhidi ya watu Wayahudi –** ***mambo yaliyofanywa kwa sura ya jina la Kristo, lakini siyo kwa tabia au haiba ya Kristo. Tuanlo jukumu katika siku zetu kuyaweka sawa yale ambayo mababa zetu waliyakosea, kwa sisi kuomba kikamilifu ili Mungu amimine baraka zake juu ya ardhi hii na watu wake.***

**Kazi hii imetafsiriwa na Askofu Daniel & Debra Ouma – DPPJ, Musoma, Tanzania.**